## KAMA UNAHITAJI USAIDIZI

Kwa hali ya haraka kwa hatari ya maisha piga simu **000**

Kama nyumba yako imeharibika vibaya sana na unahitaji usaidizi, piga simu SES nambari **132 500**.

Wanaojitolea kutoka SES watahuduria haraka iwezekanavyo. Usaidizi imepangwa kwa jambo iliyo muhimu zaidi kwanza, tafadhali kuwa na subira.

## KUSAFISHA

- Anza kusafisha mazunguko ya nyumba yako- rundika vitu ambavyo zimelegalega kama vila matawi na mabaki ya uchafu mbali na mita ya maji, vilango na laini ya simu
- Piga simu kwa serekali ya eneo yako kupata ushauri kuhusu kuondoa takataka ya matawi na vitu vingine kama vile ua ya kuzingira asbestos

## HUDUMA ZA HARAKA YA KIMATAIFA

Wanaojitolea kutoka FESA State Emergency Service (SES) wanasaidia jamii kutoka magharibi ya Australia wakati wa dhoruba na hatari mengine ya kawaida na ya kighafula.

Wanaojitolea kutoka SES wanasaidia jamii kwa:

- Kufanya Marekebisho ya mudi mfupi kwa vyumba na mabiashara. Ni jukumu yako kupanga kufanya marekebisho ya kudumu. Wasiliana na kampuni ya bima yako
- Kuondoa miti zilizoanguka
- Kuokoa watu ambao wamekwama au wamejeruhiwa
- Kuweka mifuko ya mchanga kwenye sehemu ambazo sina hatari ya mafuriko
- Kusaidia kwa kukutanisha watu tena

Usaidizi hii kwa kawaida ni duni kwa sehemu ambazo zimejitayarisha vizuri kwa wakati ambazo ni ya dhoruba, ndio sababu ambayo wanaojitolea kutoka SES wanabidii ya kuwaelimisha jamii njia ya kupungunza athari ya dhoruba kwa maisha na vyumba. Kikundi ya watu hawa ambao wamejitolea hawapati malipo na wanatoa masaa yao, kwa ujasiri wakati wa baridi, mvua, mawimbi na katika hali hatari kwenda kusaidia ma mia ya watu wanaohitaji usaidizi wa haraka.

Wakati wa dhrouba mbaya sana, kuna simu zinazopigwa nyingi zinazohitaji usaidizi ya haraka, kwa hivyo simu zinapangwa kulingana na iliyo ya muhimu zaidi kwanza. Wanaojitolea kutoka SES watahudhuria haraka iwezekanavyo.

## NAMBARI ZA SIMU ZA HARAKA

| | |
|---|---|
| Polisi. Moto, Gari ya wagonjwa (ya haraka kwa hali inayotisha maisha) | 000 |
| Huduma za usaidizi ya haraka kimataifa (SES) | 132 500 |
| Western Power | 131 351 |
| Horizon Power | 132 351 |
| Water Corporation | 131 375 |
| Alinta gas emergencies and faults (Huduma ya haraka ya Gesi na itilafu ya gesi) | 131 352 |

## KUTAFUTA MAELEZO ZAIDI

| | |
|---|---|
| Mtandao wa Fesa | www.fesa.gov.au |
| hali ya hewa kwa onyo ya dhoruba na ushauri (MOB) | 1300 659 213 |
| Kukisiwa hali ya anga na dhoruba | www.bom.gov.au |
| Hali za barabara (Barabara kuu Australia Magaribi) | 138 138 |


Mawaidha na maelezo zaidi inapatikana katika mtandao wa FESA katika lugha ya Chin, Dinka, Farsi, Vietnamese, Mandarin, Arabic, Indonesian, Somali, Swahili, French, Cantonese, Amharic, Nuer, Karen, Dari, Kirundi, Sudanese Arabic.
**Nenda mtandao: www.fesa.wa.gov.au**

*Maelezo katika mwongozo hii imetolewa na Fire and Emergency Services Authority (FESA) kwa kujitolea kama huduma ya umma. Mwongozo hii imetayarishwa kwa imani nzuri na imetolewa mahala ambazo zimeaminiwa kuwa inatumainiwa na ni sahihi kwa wakati wa chapisho. Hata hivyo, kutumainiwa na usahihi wa maelezo haiwezi kudhaminiwa na FESA inasisitiza kujitoa katika lawama yeyote kwa matokeo yeyote au kwa ukosefu ambalo imetekelezwa au imekosa kutelelezwa kwa kutegemea maelezo haya na kwa jambo lolote litokealo kwasababu yake kulingana moja kwa moja au siyo moja kwa moja kwa ajili ya tukio hii au kwa ukosefu. Kijitabu hii imekusudia kama mwongozo pekee yake na wasomaji wanapaswa kupata mawaidha yao ya kujitawala na kujitafutia maelezo inayoahitajika. Mwezi wa nne 2010*

FESA
FESA House, 480 Hay Street Perth, Western Australia 6000
GPO Box P1174, PERTH WA 6844
Simu: +61 8 9323 9300 Feksi: +61 8 9323 9384
Barua Pepe: fesa@fesa.wa.gov.au
Mtandao: www.fesa.wa.gov.au

Swahili

# KUJITAYARISHA DHORUBA





Government of **Western Australia**
**Fire & Emergency Services Authority**

FESA

## WAKATI WA DHORUBA

Dhoruba inaweza kuleta mvua nzito, mawimbi ya kuharibu, radi, mvua ya mawe,mafuriko na kimbunga kwa sehemu nusu ya kusini ya magharibi ya Australia kati ya mwezi wa tano (May) na mwezi wa kumi (October) kila mwaka. Hata hivyo dhoruba inaweza kuwa katika miezi za joto kwa hivyo ni muhimu kuwa tayari wakati wote katika mwaka.

## NINI MAANA YAKE DHORUBA?

Dhoruba inatengenezwa wakati hewa yenye joto na yenye nyevu iliyo karibu na ardhi inasukumwa upesi juu katika anga isiyo imara.

## KWA NINI KUJITAYARISHA KWA DHORUBA?

Mawimbi ya kuharibu, mafuriko ya kumulika, radi, mvua ya mawe, na kimbunga inaweza kuharibu vyumba, magari na mazingira. Zinaweza pia kuleta ajali na kupoteza maisha

Uharibivu mengi kutokana na Dhoruba inatokana na:

- vitu ambavyo vimelegalega au vitu kutoka kwa paa ambazo zimevunjika
- miti na matawi ambazo zimeanguka
- mfuriko kutoka kwa mchirizi ambazo zimefungika na bomba zilizo chini

Watu wanaweza kuwa salama na kupunguza madhara kwa nyumba yao kwa kujiweka tayari.

## VILE UNAVYOWEZA KUJITAYARISHA

Kutayarisha familia na nyumba yako kutokana dhoruba ni jukumu yako. Kama unaishi katika sehemu ambazo ni sehemu za dhoruba, unahitaji kama jambo ya kutangulia kuweka ndani na nje ya nyumba yako tayari kati ya mwezi wa tatu (March) au mwezi wa tano (May). kuna hatua chache ambazo zinaweza kusaidia kupunguza madhara:

- Angalia kama paa na mchirizi yako imeharibika au ina vitu vya kulegalega
- Ondoa matawi na vitu ambazo zimeziba mchirizi na bomba za chini
- Sawazisha au kata matawi zilizo karibu na nyumba yako na kodisha mfanyi kazi kwa mkataba kuondoa miti kutoka kwa laini za kupitisha moto
- Ondoa takataka kwenye yadi, baraza ya juu yako au weka vyombo vyovyote ambazo zimelengalenga
- Tayarisha chombo ya kuweka vitu ya haraka na kighafula iliyo na na redio ya mkono, tochi, akiba ya betri, tayarisha chombo ya vitu ya usaidizi ya kwanza na mpango wa kufuatwa na familia wakati wa haraka na kighafula
- Hakikisha familia yako inaelewa dhoruba na hatari yake
- Tayarisha mpango wa kufuatwa wakati wa haraka na kighafula ikiwa pamoja na mpango wa mahali ya kukutana ikiwa nyumba yako itagaharika. Fikiria jambo la kufanya na kipenzi (pet) yako na jua namna ya kufunga sehemu zakutoa gesi, moto, na maji (angalia mtandao wa FESA kwa maelezo zaidi)
- Onyesha wazi orodha ya nambari za simu za haraka
- Angalia kuwa una bima ya kutosha ya nyumba na vyombo

## ONYO YA HALI YA ANGA

Unaweza kuwa na habari ya kisasa kuhusu onyo ya kisasa ya dhoruba na mawaidha:

- kupitia tangazo ya habari kwenye redio, televisheni au interneti
- katika mtandao wa FESA www.fesa.wa.gov.au
- katika mtandao ya hali ya hewa (Burea of Meteorology) **www.bom.gov.au** – au kwa kupiga simu kwa laini yao ya simu ya kutoa onya ya hali ya anga ya ardhi na ushauri wa onyo ya mafuriko nambari **1300 659 213**


## WAKATI DHORUBA IMEKISIWA

- Weka salama au ondoa vitu ambavyo zimelegalega na takataka kutoka mazunguko ya nyumba yako au kazini kwasababu mawimbi yenye nguvu wakati wa dhoruba inaweza kufanya vitu ambavyo zimelega lega kuwa silaha hatari
- Tumia mifuko za plastiki zilizojazwa na mchanga ili kutia uzito kwa vitu ambazo zimelegalega badala ya kutumia matofali ambazo zinaweza kupurushwa na upepo mkali
- Hakikisha chombo yako yenye vitu vya haraka na kighafula ni ya kisasa
- Hakikisha kipenzi na wanyama wako wako katika sehemu iliyo salama
- Weka gari yako palipofunikwa
- Kama hauko nyumbani, unahitaji kuwasiliana na familia au marafiki kuhakikisha nyumba yako iko salama
- Wafanyi kazi mahala za ujenzi wanahitaji kuweka vyombo vyovyote vya ujenzi ambazo zinalegalega na kuweka kibanda yao salama
- Wenye boti wanahitaji kuhakikisha kuwa boti yao imefungwa salama
- Wenye kupiga kambi wanahitaji kutafuta kimbilio mengine

Chakula spesheli na madawa za tiba zinaweza kuhitajiwa kwa mtoto mdogo, wazee au walemavu katika familia

**CHOMBO CHA VITU VYA HARAKA NA KIGHAFULA**



## WAKATI WA DHORUBA

- Funga pazia yako na kaa ndani mbali na madirisha
- Kama umepatikana nje tafuta mahali salama mbali na miti, laini ya stima/umeme, vyombo vya chuma, malindi ya dhoruba ya kuondoa maji na mito
- Kama uko kwenye boti, unaongelea au uko katika povi ya mawimbi ondoka kwenye maji
- Kama kuna radi, ondoa vyombo zinazotumia moto kwenye tudu la kupitisha moto na usitumie simu za nyumba za laini ya ardhi
- Kama kuna mfuriko, unaweza kutengeneza mfuko wako wa mchanga kwa kutumia mfuko wa plastiki au mfuko wa mto (Pillow) iliyojazwa na mchanga
- Kama unaendesha gari kwenye mvua nzito, kuwa mwaangalifu zaidi barabarani:
  - punguza mwendo, washa mataa yako na weka umbali salama kati yako na madereva wengine
  - Kama hauwezi kuona vizuri, ondoka barabarani na egesha gari, weka mataa yako ya hatari (Hazard) hadi wakati mvua itakapoisha
  - Usiendeshe katika maji ambazo haujui kina yake na nguvu ya mkondo wa maji

## BAADA YA DHORUBA

- Pima nyumba na mali yako kuangalia madhara
- Angalia marafiki au majirani kama wanahitaji usaidizi
- Weka Watoto mbali na mfuriko wa maji, mito na njia za maji
- Epuka laini ya moto ambazo zimeanguka, kwasababu zina hatari na kwa wakati wote zichukulie kuwa bado zina moto wakati wote
- Jihadhari na miti ambazo zimeanguka na mijengo zilizoharibika
- Kama unaendesha gari, punguza mwendo, weka umbali ya salama kati yako na madereva wengine na kuwa mwaangalifu kwa sehemu ambazo zimegharika
- Kama barabara zimegharika, usiendeshe kwenye maji usiyo jua kina na nguvu yake
- Epuka barabara ya changarawe kwasababu upande wa nje itakuwa yakuteleza na yenye matope, na magari inaweza kukwama